

## UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Ndugu Mwananchi,**

Ninayo furaha kubwa kukuletea Ripoti yangu inayohusu ukaguzi nilioufanya katika Serikali Kuu ikijumuisha Wizara, Idara na Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Miradi ya maendeleo pamoja na Ukaguzi wa Ufanisi kupitia Toleo hili Maalum la Mwananchi. Ofisi yangu ya Taifa ya Ukaguzi imekuwa ikitoa toleo hili kila mwaka kwa kuzingatia mahitaji ya kitaaluma INTOSAI P12.

Lengo kuu la toleo hili ni kukushirikisha wewe, mwananchi, katika mchakato wa ukaguzi unaofanywa na Ofisi yangu kwa kukupa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi. Tunaamini kuwa kwa kukupatia taarifa hizi, tunaimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma na kukupa fursa ya kutimiza wajibu wako chini ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano (1977).

Katika toleo hili, pamoja na kaguzi zingine, pia utapata matokeo ya kaguzi za mifumo. Ninakusihi kusoma kwa umakini ili uweze kushirikiana nasi katika kusimamia rasilimali za umma.

## Wito kwa Wananchi

Ninawaomba wananchi wote kutumia taarifa zilizopo katika ripoti hii kwa lengo la kusimamia rasilimali za umma kwa ufanisi. Tafadhali toa maoni na mapendekezo yako ya kuhusu jinsi ya kuboresha utendaji wa NAOT. Kwa kushirikiana pamoja, tunaweza kujenga taifa lenye uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Asanteni sana kwa ushirikiano wenu.



Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Ripoti hii ina sura nane zinazojumuisha ukaguzi za hesabu, ukaguzi wa kiufundi, ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA uliofanyika katika sekta mbalimbali za umma katika mwaka wa fedha wa 2022/23. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii:

**Hati za Ukaguzi:** Nimetoa jumla ya hati 1209 za ukaguzi, zikijumuisha hati zinazoridhisha, hati zenye shaka, hati mbaya na hati za kushindwa kutoa maoni. Katika hati zilizotolewa zote asilimia 99 zilionesha kuridhisha, ishara inayoonesha kuwa utayarishaji wa hesabu umezingatia kwa kiwango kikubwa matakwa ya viwango vinavyotumika.

**Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi:** Ripoti inaonesha kuwa alimia 41 ya mapendekezo yaliyotolewa yametekelezwa kikamilifu, asilimia 10 hayajatekelezwa, huku 38% bado yakiendelea kutekelezwa, asilimia 7 yaliyojirudia na asilimia 4 yaliyopitwa na wakati. Hata hivyo, bado kuna nafasi ya kuboresha katika baadhi ya maeneo, kwa lengo la kuhakikisha mapendekezo yote yanafanyiwa kazi.

Ripoti inajumuisha matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, na Miradi ya Maendeleo, pamoja na ukaguzi wa ufanisi na mifumo ya TEHAMA. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na:

- Shilingi bilioni 42.92 zimetumika katika shughuli ambazo hazikuwa kwenye bajeti ama kulipa kwa kutumia vifungu vya matumizi visivyo sahihi
- Fedha zilizobadilishwa matumizi bila idhini ya mamlaka husika Sh. bilioni 4.88
- Malipo ya Shilingi bilioni 2.95 kwa kazi ambazo hazijapimwa au hazijatekelezwa

- Mapato ya Shilingi bilioni 72.89 yasiyokusanywa na Shilingi bilioni 6.18 yasiyowasilishwa benki hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo
- Miradi isiyokamilika, na iliyokamilika lakini haitumiki
- Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kutoa fedha pungufu kwa kwa ajili ya elimu bila malipo kiasi cha Shilingi bilioni 1.25
- Matumizi yasiyokuwa na tija ya shilingi bilioni 224.46
- Gharama za ziada Shilingi bilioni 130.51 katika miradi ya Barabara
- Kutokamilika kwa miundombinu hivyo kukwamisha matumizi ya miradi ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.66
- Uhaba wa wataalamu, miundombinu, vifaa tiba, na dawa katika vituo vya afya



# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI




## 1.1 Utangulizi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi kuu ya ukaguzi nchini yenye jukumu la kukagua mapato na matumizi ya Serikali, kama yanavyoidhinishwa na Bunge na kutoa taarifa ya ukaguzi Bungeni. Ofisi hii inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambaye majukumu yake yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (*kama ilivyorekebishwa*); Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 na Kanuni zake za Mwaka 2009, pamoja na Sheria nyingine.

## 1.2 Usimamizi wa Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji

**Bunge**

Kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali pamoja na kutunga sheria za usimamizi za Umma

**Serikali**

Kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyoidhinishwa na Bunge

**Mahakama**

Kutafsiri Sheria kwa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa Mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria za nchi

## 1.3 Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

- Kuidhinisha malipo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali baada ya kuhakikisha fedha zinazokusudiwa kutolewa malipo yake yamepata kibali na yameidhinishwa na Bunge.
- Kuhakikisha matumizi ya fedha yatokanayo na fedha kutoka mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali yametumika kwa Malengo yaliyokusudiwa.
- Kufanya Ukaguzi na kutoa taarifa ya Ukaguzi wa hesabu za Serikali, Mahakama, na Bunge angalau mara moja kila mwaka.
- Majukumu na kazi zake zimefafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 5,9,10 na 11 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008.


KUFANYA UKAGUZI NA KUTOA TAARIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIHIMILI MITATU YA DOLA..

HATI ZA UKAGUZI

# SURA YA PILI

# HATI ZA UKAGUZI WA HESABU NA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

## 2.1 Hati za Ukaguzi

Hati ni maoni ya ukaguzi yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika ukaguzi wa taarifa za fedha endapo zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (kama vile IFRS au IPSAS). Maoni haya hutolewa kwa kuzingatia tathmini ya vielelezo vinavyopatikana wakati wa ukaguzi. Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) 1700. Kuna aina nne za Hati za Ukaguzi ambazo ni Hati inayoridhisha, Hati yenye shaka, Hati mbaya na Hati ya kushindwa kutoa maoni.

# Hati za Ukaguzi

## Hati inayoridhisha

Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaporidhika kuwa taarifa za fedha alizokagua zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango kubalifu vya kimataifa vinavyohusu uandaaji wa taarifa za fedha. Aidha, hati hii hutolewa pale Mkaguzi anapokuwa amejiridhisha kuwa mapungufu yaliyobainika hayawezi kuathiri ubora wa hesabu zilizoandaliwa

## Hati yenye shaka

Hati hii hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa, Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha wakati wa ukaguzi, akahitimisha kuwa kulikuwa na dosari ama moja moja au kwa ujumla wake, ambazo ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha. Pia hotelewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

## Hati mbaya

Hati hii hutolewa pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha kuwa dosari ama moja moja au kwa ujumla zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kubwa na zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi.

## Kushindwa kutoa maoni


Hati hii hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha utakaomuwezesha kutoa maoni ya ukaguzi; Mkaguzi atahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea za dosari zisizogundulika katika taarifa za fedha, zinaweza kuwa kubwa na zinaweza kuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

## 2.2 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Katika mwaka huu, nimetoa jumla ya **hati 1,209 za ukaguzi**, zikihusisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Serikali Kuu, Miradi ya Maendeleo na Vyama vya Siasa. Mgawanyo wa hati za ukaguzi ni kama inavyoonekana katika mchoro hapo chini: -

Hati zinazoridhisha
**1,198**
(99%)


Hati zenye shaka
8
(0.7%)



Hati mbaya
1
(0.1%)

Kushindwa kutoa maoni
2
(0.2%)

Kwa ujumla, utendaji wa taasisi za Serikali katika kuandaa hesabu umeonesha matokeo mazuri, kwani asilimia 99 ya hati zote zilizotolewa zilionesha kuridhisha.



## 2.3 Taasisi zilizopata hati zenye shaka, mbaya au kushindwa kutoa maoni

**Jedwali Na. 1** linaonesha orodha ya taasisi zilizopata hati zenye shaka, mbaya, au kushindwa kutoa maoni.

**Jedwali Na. 1: Taasisi zilizopata hati zenye shaka, mbaya na kushindwa kutoa maoni**


| Na. | Taasisi | Aina ya Hati |
|---|---|---|
| **SERIKALI ZA MITAA** | | |
| 1. | Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti | Yenye shaka |
| 2. | Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe | Yenye shaka |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi | Yenye shaka |
| **MASHIRIKA YA UMMA** | | |
| 4. | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (TSN) | Yenye shaka |
| 5. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) | Yenye shaka |
| 6. | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) | Yenye shaka |
| 7. | Bodi ya Nyama Tanzania (TMD) | Yenye shaka |
| **SERIKALI KUU (CBWSO's)** | | |
| 8. | Chombo cha Watoa Huduma ya Maji Utegi | Kushindwa Kutoa Maoni |
| **VYAMA VYA SIASA** | | |
| 9. | Civic United Front (CUF) | Yenye shaka |
| 10. | National Reconstruction Alliance (NRA) | Mbaya |
| 11. | Alliance For African Farmers Party (AAFP) | Kushindwa kutoa maoni |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| 12. | Mradi wa kujumuisha malengo katika kupambana na athari za Mazingira, Umaskini na Jinsia katika Kuleta Maendeleo Endelevu na Kuondoa Umaskini | Yenye shaka |




## 2.4 Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi

Katika ripoti zilizopita, nilitoa mapendekezo kadhaa yaliyokusudia kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma na kuboresha ukusanyaji wa mapato kama inavyoonekana hapo chini.

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi




Ingawa kuna maendeleo katika utekelezaji wa mapendekezo, bado kuna nafasi ya kuboresha katika baadhi ya maeneo. Asilimia 41 tu ya mapendekezo yote yametekelezwa kikamilifu, na asilimia 38 bado yanaendelea kutekelezwa. Asilimia 10 ya mapendekezo hayajaanza kutekelezwa hata kidogo, na asilimia 4 yamefutwa kwa sababu ya kupitwa na wakati.



## 2.5 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Katika Ukaguzi za Ufanisi

Mchoro unaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi 12 za ufanisi zilizowasilishwa Bungeni mwaka 2023.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo katika kaguzi za ufanisi




Utekelezaji wa mapendekezo bado hauko katika kiwango cha kuridhisha kwani ni mapendekezo 30 sawa na asilimia 22 tu yaliyotekelezwa kikamilifu, wakati mapendekezo 79 sawa na asilimia 58 hayajatekelezwa kikamilifu na mapendekezo 28 sawa na asilimia 20 hayakutekelezwa kabisa.



# SURA YA TATU

# UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU

## 3.2 Mwenendo wa deni la serikali

Kufikia tarehe 30 Juni 2023, deni la serikali lilifikia Sh. trilioni 82.25, sawa na ongezeko la Asilimia 15 kutoka Shilingi trilioni 71.31 mwaka 2021/22. Deni hilo linajumuisha deni la ndani la Sh. trilioni 28.92 na deni la nje la Sh. trilioni 53.32. Hata hivyo, kipimo cha deni la serikali kinachotumia pato la taifa (GDP) kinaonesha kuwa deni ni himilivu.




## 3.3 Kukosewa kwa ukokotoaji wa mafao na waajiri

Ukaguzi wa majalada ya mafao ulibaini kuwa kati ya majalada 2,873 yaliyoidhinishwa kwa malipo, majalada 41 (1%) yalikokotolewa kimakosa. Hata hivyo, makosa hayo yalirekebishwa na malipo kuidhinishwa. Majalada 23 (56%) yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa jumla ya Sh. milioni 110.05 na majalada 18 (44%) yalikokotolewa kwa kiwango pungufu kwa jumla ya Sh. milioni 138.78. Hata hivyo, makosa hayo yalirekebishwa na malipo kuidhinishwa.

Makosa hayo yalitokana na kurekodi kipindi kisicho sahihi cha utumishi, kukokotoa mafao kwa kutumia mishahara na michango ya watumishi isiyo sahihi na makosa ya majumuifu.

**Mafao yaliyokosewa katika ukokotoaji**




## 3.4 Usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi

Ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, umebaini makusanyo ya jumla ya Shilingi trilioni 22.58 kwa mwaka wa fedha 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia nane ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 20.94 mwaka 2021/22. Licha ya ongezeko hilo, makusanyo hayo yalikuwa chini kwa Sh. trilioni 1.07, sawa na asilimia 4.5 ya makadirio ya awali.

## 3.5 Mafuta yasiyotozwa ushuru kwa kupitiliza muda wa kukaa nchini

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa mafuta yenye thamani ya Sh. milioni 929.6 yaliyokusudiwa kwenda nchi jirani yaliyopitiliza muda wa kukaa nchini kwa muda wa zaidi ya siku 30 lakini hayakutozwa ushuru wa forodha.

## 3.6 Kutokuhakikiwa kwa mita za maji

Katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa mita za maji 15,827 za taasisi 32 za kijamii za utoaji wa huduma za maji hazikuhakikiwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo (WMA). Hali hii inaweza kusababisha wateja kutozwa ankara zisizo sahihi au kusababisha upotevu wa mapato kwa upande mwingine.

## 3.7 Mapato yaliyokusanywa nje ya mifumo ya makusanyo

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mapato ya Shilingi bilioni 7.73 yalikusanywa nje ya mifumo ya makusanyo ya Serikali, kinyume cha sheria na sera zilizopo. Aidha, Taasisi tatu za Serikali zilikusanya mapato bila kutumia namba za udhibiti wa malipo (Control number) na mifumo ya makusanyo kama ifuatavyo:

(i) Wizara ya Elimu (Fungu 46): Shilingi bilioni 3.99
(ii) Taasisi za watoa huduma ya maji: Shilingi bilioni 3.01
(iii) Wizara ya Uvuvi (Fungu 64): Shilingi milioni 730.51

Kutotumiwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kunaweza kuleta athari za upotevu na ubadhirifu wa mapato, hivyo kuongeza nakisi ya bajeti.

## 3.8 Kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba

Nimebaini uchelewaji wa kuanza kwa utekelezaji wa mikataba yenye thamani ya Shilingi bilioni 302.01. Hili limebainika katika Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA). Hii inahatarisha utoaji wa huduma muhimu kwa jamii, kuongezeka kwa malalamiko kutoka kwa watumiaji wa miradi.



# SURA YA NNE

# UKAGUZI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## A. UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA BAJETI

### 4.1 Fedha za miradi zilizochepushwa kutumika kwenye miradi mingine pamoja na shughuli za kawaida ambazo hazikukusudiwa kiasi cha Shilingi bilioni 7.73

Nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za mitaa 26 zilielekeza Shilingi bilioni 7.73 katika kutekeleza miradi na matumizi ya kawaida ambayo hayakuwa sehemu ya mpango uliokusudiwa awali. Uchepushaji huu wa fedha unadhihirisha kwamba shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa, hivyo kuathiri uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutoa huduma bora kwa jamii.

### 4.2 Fedha zilizobadilishwa matumizi bila kuidhinishwa na mamlaka husika kiasi cha Shilingi bilioni 4.88

Nimebaini kuwa Mamlaka za serikali za mitaa nne (H/W Mpimbwe, H/M Sumbawanga, H/Jiji Dodoma na H/Jiji Mwanza) zilibadilisha matumizi ya fedha za miradi bila idhini, zikitumia Shilingi bilioni 4.88 kinyume na sheria ya bajeti, hali iliyosababisha matumizi bila kuzingatia malengo ya bajeti iliyoidhinishwa na kusababisha uvunjaji wa kanuni za uwajibikaji wa kifedha.




## 4.3 Malipo ya Shilingi bilioni 3.04 kwa kazi ambazo hazijapimwa au hazijatekelezwa

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Mamlaka za serikali za mitaa 12 zilizolipa jumla ya Shilingi bilioni 3.04 kwa kazi zilizotekelezwa bila kuwepo kwa nyaraka zinazoonesha ukubwa wa kazi (*measurements*), na mamlaka tano zililipa Shilingi milioni 408.69 kwa kazi zisizotekelezwa, kutokana na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha wa miradi. Hii inakwamisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa malipo hasa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## B. USIMAMIZI WA MAPATO

### 4.4 Mapato ya Shilingi bilioni 72.89 yasiyokusanywa na 6.18 yasiyowasilishwa benki yanayokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Katika jitihada za kuboresha usimamizi wa mapato na kuhakikisha ufanisi katika mamlaka za serikali za mitaa, ukaguzi umebaini kuwa halmashauri hazikukusanya kiasi cha  Shilingi bilioni 67.24 kutoka katika vyanzo vikubwa muhimu wakati Shilingi 11.83 zilizokusanywa hazikuwasilishwa benki. Hali hii inaathiri uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza miradi ya maendeleo na kutoa huduma bora kwa jamii.

- Mapato yasiyokusanywa kutoka vyanzo muhimu ya Shilingi bilioni 61.15 yalibainika katika mamlaka 130 za serikali za mitaa kutokana na udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mapato.

- Mapato ya Shilingi bilioni 6.18 yaliyokusanywa kupitia mashine za POS hayakuwasilishwa katika akaunti za benki za mamlaka 96 za serikali za mitaa.

- Ukusanyaji usioridhisha katika vyanzo vikubwa vya mapato ulibainika kwa makusanyo kufikia Shilingi bilioni 1.94 tu kati ya makadirio ya Sh. bilioni 8.03 kutoka vyanzo vikubwa vya mapato katika mamlaka nne za serikali za mitaa wakati kiasi cha Shilingi bilioni 6.09 hakikukusanywa kabisa.

- Mapato yasiyowasilishwa na mawakala yalionesha kuwa, Mamlaka 12 za serikali za mitaa zilipata Shilingi bilioni 8.88 pekee kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji, huku Shilingi bilioni 5.65 zikiwa hazijawasilishwa kulingana na mikataba.

### 4.5 Mapato ya ndani kiasi cha Shilingi bilioni 20.23 mbayo hayakutengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za vijiji/mitaa

Mamlaka 184 za serikali za mitaa hazikutenga jumla ya Shilingi bilioni 20.23 za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shughuli za uendeshaji. Hii inajumuisha Shilingi bilioni 17.60 za miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 2.63 zilizotakiwa kutumika kwa uendeshaji wa shughuli za vijiji/mitaa, kilimo, uvuvi, ufugaji na ufadhili wa miundombinu ya barabara kupitia TARURA. Hii inatokana na halmashauri nyingi kushindwa kukusanya mapato kutoka katika vyanzo muhimu.

## C. MATUMIZI NA MISHAHARA

### 4.6 Matumizi yasiyo sahihi ya Shilingi Bilioni 7.11 katika akaunti za amana

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa matumizi yasiyo sahihi ya Sh. bilioni 7.11 kutoka kwenye akaunti za amana (**Deposit Accounts**). Malipo haya yalifanyika kinyume na malengo yaliyokusudiwa ya fedha zilizowekwa katika akaunti ya amana, na kusababisha athari hasi kwenye uwezo wa mamlaka husika kutekeleza miradi na shughuli zilizopangwa.



Kwanza Shilingi bilioni 5.16 zilitumika kwa shughuli zisizokusudiwa na fedha hizo hazikurejeshwa kwenye akaunti husika. Pili, mamlaka 17 za serikali za mitaa zilifanya malipo yanayozidi kiasi kilichowekwa kwenye akaunti za amana kwa jumla ya Shilingi bilioni 1.95.

### 4.7 Makato ya kisheria katika mishahara ya Shilingi bilioni 36.08 kutowasilishwa katika taasisi husika

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka za serikali za mitaa 46 pamoja na kukata makato ya kisheria katika mishahara, hazikuwasilisha makato hayo ya Sh. bilioni 36.08 katika taasisi husika kama PSSSF na NHIF, ikiwa ni pamoja na kutozwa faini ya Sh. bilioni 32.08 kwa kuchelewesha michango. Hali hii ina athari katika utoaji wa mafao ya kustaafu na husababisha matumizi yasiyokuwa ya lazima ya fedha za serikali.

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### 4.8 Miradi isiyokamilika, iliyotelekezwa na iliyokamilika lakini haitumiki

Nimebaini kuwepo kwa Miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 20.24 iliyotelekezwa, Shilingi bilioni 11.21 iliyokamilika lakini haitumiki na Shilingi bilioni 272.88 isiyokamilika. Matokeo haya yanaashiria changamoto kubwa katika usimamizi na utekelezaji wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa, pamoja na athari za ufinyu wa bajeti unaosababisha miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 20.57 kutotekelezwa.

## E. SEKTA YA ELIMU

### 4.9 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kutoa fedha pungufu kiasi cha Shilingi bilioni 1.25 kwa ajili ya elimu bila malipo

Nimebaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutoa Shilingi bilioni 1.25 za ruzuku ya elimu bila malipo kwa mamlaka 15 za serikali za mitaa, ikilinganishwa na mahitaji ya Shilingi bilioni 11.83, kwa mujibu wa waraka wa ruzuku. Hii imeathiri upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, ukarabati wa miundombinu, na hivyo kudhoofisha mazingira ya elimu.

## F. SEKTA YA AFYA

### 4.10 Vifaa tiba vilivyonunuliwa na sehemu za huduma za afya zilizokamilika lakini hazitumiki zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.94

Nimebaini kuwa Mamlaka 10 za Serikali za Mitaa zilinunua vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 2.42 ambavyo havikuanza kutumika kwa sababu ya kutokukamilika kwa baadhi ya majengo ya afya, ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi, na masuala ya kiufundi. Vilevile, mamlaka 6 zilikamilisha ujenzi wa majengo ya afya yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.52, ambayo hayatumiki ipasavyo au hayatumiki kabisa, kutokana na ukosefu wa rasilimali kama vile samani, umeme, na maji.



### 4.11 Kuchelewa kupokelewa kwa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 1.78 Kutoka MSD

Mamlaka 15 za Serikali za Mitaa zililipa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) jumla ya Shilingi bilioni 3.05 kwa ajili ya kununua vifaa tiba, lakini bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.78 kwa muda mrefu hazikupokelewa kwa muda mrefu hadi wakati wa ukaguzi, ikiwa ni asilimia 58 ya malipo.

## G. SEKTA YA UWEKEZAJI

### 4.12 Hasara ya Shilingi bilioni 22.37 iliyotokana na uwekezaji usio na tija

Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mkoa wa Dar es Salaam zilizowekeza Shilingi bilioni 26.89 katika Benki ya DCB zimepata hasara ya Shilingi bilioni 22.37 kutokana na kupungua kwa thamani ya hisa zake. Ukaguzi umeonesha kuwepo kwa utendaji mbaya wa uwekezaji pamoja na ukwasi usioridhisha wa benki uliopelekea kushindwa kutangaza gawio kwa zaidi ya miaka minne.

Pia, uwekezaji kwenye hisa za kampuni nyingine kama TCC, TCCL na TBL umekuwa na matokeo yasiyoridhisha, yakiambatana na kuchelewa kwa malipo ya gawio.

### 4.13 Mapungufu katika uendeshaji wa timu za mpira wa miguu za Mamlaka za Serikali za Mitaa

Timu nne za mpira wa miguu zinazomilikiwa na mamlaka za Serikali za mitaa - KMC, Geita Gold, Mbeya City na Dodoma Jiji zinazoshiriki katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara zilipata mapato ya Shilingi bilioni 7.01 kutoka vyanzo mbalimbali, huku zikichangiwa Shilingi bilioni 3.66 na Halmashauri zao kutoka katika vyanzo vya ndani.

Ukaguzi umeonesha kuwa Halmashauri hazina miongozo wala taratibu zilizowekwa za uendeshaji wa timu hizi, ikiwemo usajili, usimamizi wa fedha, miundombinu, haki za wafanyakazi na wachezaji, pamoja na mgawanyo wa mapato. Zaidi ya hayo, vilabu hivi havikujumuishwa katika mfumo wa malipo serikalini (MUSE) na hesabu zao hazikuandaliwa wala kuwasilishwa katika mikutano ya kila mwezi ya Kamati ya Fedha. Hali hii inayoashiria ukosefu wa uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika usimamizi wa mapato na matumizi ya vilabu.

## H. SEKTA YA ARDHI

### 4.14 Mikopo ya Programu ya KKK ambayo haijarejeshwa Shilingi bilioni 21.85

Halmashauri 47 zilishindwa kurejesha mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 21.85 ya Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK). Sababu kuu ya kushindwa ni pamoja na kasi ndogo ya uuzaji viwanja kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokulipwa kikamilifu kwa fidia.



## 4.15 Mwenendo wa kesi za ardhi zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.18 dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakabiliwa na mashauri 61 yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.18 na mashauri 33 yasiyohusisha madai ya fedha, yakiashiria changamoto kubwa katika usimamizi wa ardhi. Migogoro hii inatokana na malalamiko kama vile kutwaa ardhi pasipo kulipa fidia stahiki, ukosefu wa uwazi, ugawaji wa viwanja mara mbili, na utwaaji wa ardhi usio rasmi. Kesi hizi zinaweza kuathiri rasilimali fedha za mamlaka na kuwafanya wananchi kukosa imani na Mamlaka husika.




## I. UFANISI WA SEKRETARIETI ZA MIKOA

## 4.16 Fedha za maendeleo kiasi cha Shilingi bilioni 1.04 zilizotumika kwa malengo yasiyokusudiwa na kulipwa nje ya vifungu husika

Sekretarieti nne za Mikoa zilitumia Shilingi bilioni 1.01 kinyume cha malengo yaliyokusudiwa, huku sekretarieti tatu zikitumia Sh. milioni 25 katika vifungu visivyo sahihi. Matumizi haya yasiyo ya bajeti yalikwamisha utekelezaji wa mipango iliyokusudiwa na kuonesha udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma.

### 4.17 Ucheleweshaji wa ugawaji wa bakaa ya fedha taslimu Shilingi bilioni 2.6 kutoka Halmashauri Iliyovunjwa ya Jiji la Dar Es Salaam

Nimebaini kuwepo kwa uchelewaji katika kugawa bakaa ya Shilingi bilioni 2.6 kutoka katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliyovunjwa. Hii inaashiria agizo la OR-TAMISEMI la tarehe 25 Februari 2021, lililotaka mali na madeni katika Halmashauri iliyovunjwa na Manispaa za Dar es Salaam kusimamiwa na kuratibiwa, halijatekelezwa kikamilifu.

## J. OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### 4.18 Kutokukusanya ushuru wa maegesho Shilingi bilioni 9.98

Ukaguzi wa mfumo wa ukusanyaji wa ushuru wa maegesho ulibaini kwamba, kuanzia Aprili 2021 hadi Juni 2023 wamiliki wa vyombo vya usafiri vilivyoegeshwa kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara hawakulipa kiasi cha jumla ya Shilingi bilioni 9.98 kama ushuru wa maegesho na OR – TAMISEMI haikuchukua hatua zozote thabiti kuhakikisha ukusanyaji wa kiasi hicho cha fedha.

### 4.19 Manunuzi ya Shilingi bilioni 14.81 yaliyofanyika bila kutumia njia ya ushindani wa bei

Nimebaini kuwa TARURA ilifanya manunuzi ya Shilingi bilioni 14.81 bila kutumia njia ya ushindani wa bei, kinyume na taratibu za Ununuzi wa Umma, ambazo zinahitaji zabuni kufanywa kwa uwazi na ushindani. Hali hii inapunguza uwazi na kuzuia matumizi bora ya fedha za umma.



# SURA YA TANO

# UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA


## A. UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA

### 5.1 Taasisi zilizopata hasara au nakisi

Utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma bado hauko katika hali nzuri. Juhudi zaidi zinahitajika kuboresha usimamizi, kupunguza gharama, na kuongeza mapato. Mashirika 34 yamepata hasara kwa miaka miwili mfululizo, Mashirika 11 ya kibiashara na Mashirika 23 yasiyo ya kibiashara.

Sababu za Hasara ni pamoja na gharama kubwa za uendeshaji, kupungua kwa mapato, udhaifu wa usimamizi na uwekezaji usiofaa. Kukabiliana na hali hii Serikali imechukua jitihada za kutoa ruzuku kwa baadhi ya mashirika pamoja na kufanya mabadiliko ya kimkakati kuboresha utendaji na uimarishaji wa usimamizi. Mifano ya Mashirika yaliyopata hasara ni pamoja na: -

- Shirika la Reli Tanzania (TRC): Hasara ya Shilingi bilioni 100.70
- Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL: Hasara ya Shilingi bilioni 76.56
- Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL): Hasara ya Shilingi bilioni 56.64
- Shirika la Posta Tanzania: Hasara ya Shilingi bilioni 1.34
- Kampuni ya Mawasiliano ya Tanzania (TTCL): Hasara ya Shilingi milioni 894
- Soko la Bidhaa Tanzania (TMX): Hasara ya Shilingi milioni 720




**Wito kwa Wananchi**

Tumia huduma za mashirika ya umma ili kuimarisha mapato yao

**Wito kwa Serikali**

- Kuendelea kusimamia mashirika ya umma kwa ufanisi
- Kufanya mageuzi yanayofaa kuboresha utendaji

Kwa ujumla, hali ya kifedha ya mashirika ya umma bado inahitaji maboresho makubwa. Serikali na wananchi wote wanapaswa kuchukua hatua za kuhakikisha mashirika haya yanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa manufaa ya jamii.



## B. UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA UTENDAJI KAZI

### 5.2 Ubadilishaji usio wa kawaida wa mita za umeme

Ukaguzi wa ripoti ya kubadilisha mita za umeme mwaka wa fedha 2022/23 ulibaini kuwa mita 108,088 kati ya mita 602,269 zilibadilishwa na TANESCO kabla ya kipindi cha uhai wa matumizi yake kuisha. Mita 13,493 zilibadilishwa ndani ya mwaka mmoja baada ya kufungwa kwake na mita 94,595 zilikuwa na muda mfupi wa matumizi kati ya mwaka mmoja hadi miaka 15. Kubadilisha mita mapema husababisha gharama zaidi.

### 5.3 Malipo yasiyothibitishwa kwa mzabuni

Katika mwaka wa fedha 2022/23, TANESCO ililipa dola za Marekani milioni 10.16 kwa mzabuni bila uthibitisho wa ubora wa kazi kutoka kwa mshauri elekezi. Hii ilikuwa kinyume na mwongozo wa uendeshaji wa kitengo cha uwekezaji wa TANESCO. Hali hii ilitokana na mratibu wa mradi kutekeleza majukumu mawili kwa wakati mmoja.



## 5.4 Kuchelewa Kutekeleza Miradi ya Wajibu wa Kijamii (CSR) - TANESCO

Nimebaini kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya wajibu wa kijamii (CSR), yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 262 kwa ajili ya Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP).

Katika Mradi huu, mpango wa awali ulikuwa kujenga kituo cha michezo na kuboresha barabara. Hata hivyo, hali ya kutokubaliana ilitokea kati ya TANESCO na mkandarasi kuhusu miradi husika na maeneo yake.

Hii ilisababisha mabadiliko kadhaa, yakiwemo kujenga vyuo vya ufundi katika maeneo mbalimbali.

Kwa bahati mbaya, mabadiliko haya yamesababisha kuchelewa kwa makubaliano kuhusu utekelezaji wa miradi ya kijamii. Hii inahatarisha uwezo wa mradi wa kuwapa Watanzania faida zilizopangwa.

# C. USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA

## 5.5 Mashirika manne yashindwa kuhamisha Shilingi bilioni 21.84 kwenda Benki Kuu ya Tanzania

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa mashirika manne ya umma ambayo haya kuhamisha jumla ya Shilingi bilioni 21.84 kwenda Benki Kuu ya Tanzania kama ilivyoelekezwa na Waraka Na. 3 wa 2022/23. Tumebaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilikwenda kinyume na maagizo ya bodi yake na Waraka kwa kuhamisha shilingi bilioni 19.04 kwenda akaunti ya matumizi iliyopo NMB.

## 5.6 Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo wa Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG) Shilingi bilioni 23.27

Mashirika nane ya umma yalikusanya mapato ya Shilingi bilioni 23.27 nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG). Kushindwa kukusanya mapato kupitia GePG kunaweza kusababisha upotevu wa mapato na kufifisha juhudi za udhibiti na uwazi katika mapato ya Serikali.



## D. USIMAMIZI WA MATUMIZI





### 5.7 Matumizi yasiyokuwa na tija ya Shilingi bilioni 72.36

Nimebaini kuwepo kwa Mashirika 17 ya umma yaliyotumia Shilingi bilioni 72.36 kwa matumizi yasiyo na tija katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, hili ni ongezeko la asilimia 13 kutoka mwaka uliopita wa 2021/22. Matumizi hayo yalijumuisha tozo za adhabu na riba kutokana na kuchelewesha malipo ya wakandarasi na wazabuni na kununua bidhaa zisizohitajika. Hii inasababisha upotevu wa fedha za umma na ufanisi mdogo wa matumizi ya rasilimali. Katika mashirika haya 17, Mashirika 4 yaliripotiwa katika ripoti ya mwaka jana na yamejirudia tena mwaka huu.

## E. MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI

### 5.8 Usimamizi duni wa dhamana za mikopo

Ukaguzi umebaini kuwa Benki ya Biashara Tanzania na Benki ya Azania zilitoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 410.09, wakati usimamizi wa dhamana zilizowekwa na wakopaji ulikuwa duni. Nimebaini pia kuwa baadhi ya wateja hawakuweka dhamana kinyume na matakwa ya mikataba yao ya mikopo na kwa baadhi ya mikopo kulikosekana ripoti za uthamini na bima. Hali hii inaweza kusababisha hasara kubwa kwa benki endapo wakopaji watashindwa kurejesha mikopo yao.




### 5.9 Mikopo ya Benki ya Biashara Tanzania ilitolewa kuzidi ukomo na bila kupata kibali cha Bodi ya Wakurugenzi

Ukaguzi umebaini kuwa Benki ya Biashara Tanzania ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 734.28, ambayo ilizidi ukomo bila ya kupata kibali cha Bodi ya Wakurugenzi. Mikopo hiyo ilikuwa juu ya ukomo ulioidhinishwa katika Sera ya Benki na ilitolewa kwa sekta ambazo hazijaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Jambo hili linaweza kuipeleka Benki kupata hasara.



SURA YA SITA

# UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

## 6.1 Waathirika 567 wa miradi hawakulipwa fidia kiasi cha Shilingi bilioni 13.69

Fidia ya Shilingi bilioni 13.69 haikulipwa kwa watu 567 walioathirika katika miradi sita iliyotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 12.23 kinahusisha Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Kenya na Tanzania (KTPIP) na Sh. bilioni 1.02 kilikuhusu ya mradi wa Maendeleo wa Nishati ya Jua Tanzania. Licha ya miradi minne kukaribia kukamilika (97% hadi 100%), malipo ya fidia hayakufanyika hadi wakati wa ripoti hii.



## 6.2 Gharama za ziada za miradi ya Barabara - Shilingi bilioni 130.51

Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, nilifanya ukaguzi wa kiufundi wa udhibiti wa gharama katika ujenzi wa miradi mitano ya barabara chini ya TANROADS. TANROADS ilitumia gharama kubwa ya Shilingi bilioni 130.51 katika miradi sita kutokana na mapungufu katika upembuzi yakinifu, dosari katika usanifu, usimamizi mbovu wa mikataba, na kucheleweshwa kwa miradi na malipo ya wakandarasi na washauri elekezi.

Mapungufu katika upembuzi yakinifu yalipelekea ongezeko la gharama la Shilingi bilioni 44.97 sawa na asilimia 34 ya gharama zote za ziada. Ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi na washauri ulisababisha gharama za riba ya Shilingi bilioni 85.53 sawa na asilimia 66 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Nyongeza ya gharama katika miradi iliyotekelezwa na TANROADS**

| Mradi | Tatizo Lililobainika | Ongezeko la Gharama (Sh. Bilioni) |
|---|---|---|
| Mikumi-Kidatu, Kikusya-Matema, Mpemba-Isongole, Wami Bridge, Maswa-Mwigumbi | Upembuzi yakinifu kushindwa kuonesha vizuri hali za udongo, eneo na maji | 44.97 |
| **Jumla ndogo** | | **44.97** |
| Mikumi -Kidatu, Kikusya-Matema, Mpemba-Isongole, Wami Bridge, Maswa -Mwigumbi | Ucheleweshaji katika kukamilika kwa mradi | 29.87 |
| Kikusya–Matema, Mpemba–Isongole, Daraja la Wami, Maswa–Mwigumbi | Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi na washauri uliopelekea riba | 42.8 |
| Mikumi-Kidatu, Kikusya-Matema, Mpemba-Isongole, Wami Bridge, Maswa-Mwigumbi | Marekebisho ya bei za mkataba na gharama zilizotokana na kucheleweshwa kwa miradi | 8.88 |
| Barabara ya Mikumi- Ifakara | Malipo bila mkataba | 3.99 |
| **Jumla ndogo** | | |
| **Jumla** | | |

## 6.3 Riba kutokana na Kuchelewesha Malipo na Usimamizi Duni wa Mikopo Shs. Bilioni 224.47




Ukaguzi wangu umebaini matumizi mabaya ya fedha za umma katika taasisi mbalimbali za serikali, yaliyosababisha hasara ya zaidi ya Shs bilioni 224.47. Hasara hii imetokana na kuchelewesha malipo kwa wakandarasi na usimamizi duni wa mikopo, na hivyo kusababisha malipo makubwa ya riba.

Gharama hii imegawanywa katika maeneo makuu mawili:

i) Kuchelewesha Malipo kwa Wakandarasi (Shilingi Bilioni 222.34): Ukaguzi tofauti ulibaini kuwa TANROADS na TARURA ndizo zilizokuwa na mzigo mkubwa wa malipo ya riba, jumla ya shilingi bilioni 222.34. Hii ilitokana na kuchelewesha malipo kwa wakandarasi kwenye miradi 68 ya barabara. Ucheleweshaji huo uliwasababishia kuwaletea mzigo wa kifedha na kuwafanya watoze riba kwenye malipo yaliyochelewa kulingana na masharti ya mkataba.

ii) Utumiaji Duni wa Mikopo na Malipo ya kutotumika kwa Mkopo (Shilingi Bilioni 2.13): TANESCO ilibainika kusababisha hasara ya TZS bilioni 2.13 kama riba ya ziada kutokana na usimamizi mbovu wa

mikopo, ikiwemo kuchelewa kutumia fedha zilizokopwa na kukiuka makubaliano ya mkopo wa Mradi wa Usafirishaji wa Umeme kati ya Tanzania na Zambia.

Gharama hizi hazina tija kwa kuwa ni gharama ambazo zinaweza kuepukwa kwa kuhakikisha kwamba serikali inafanya malipo kwa wakati.

## 6.4 Kutokamilika kwa miundombinu kumekwamisha matumizi ya miradi ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.66

Miradi kadhaa ya serikali imekumbwa na changamoto ya kutokamilika kwa miundombinu muhimu kutokana na ukosefu wa usanifu na usimamizi bora wa miradi, pamoja na bajeti finyu . Mifano ni pamoja na:

- **Visima 15** vilivyochimbwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 9.16** katika eneo la Usa River – Makumira – Tengeru mkoani Arusha vilikosa miundombinu ya usambazaji maji.




- Majengo ya shule yenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.39** yalikamilika lakini hayakuanza kutumika kutokana na kukosa samani na maji.

- Marambo ya kunyweshea mifugo yaliyogharimu Shilingi milioni 107 hayajatumika kutokana na vikwazo vya kisheria.

## 6.5 Mapungufu katika utendaji wa injini za Vivuko

Katika ukaguzi wa TEMESA, niligundua kasoro kubwa katika utendaji na ubora wa injini za kivuko cha MV Kilindoni na MV Kazi. Kivuko cha MV Kilindoni, licha ya gharama ya Shilingi bilioni 5.07 iliyotumika katika ujenzi wake, kilishindwa kufanya vizuri katika majaribio ya baharini kutokana na joto la injini kupanda kupita kiasi. Hii ilitokana na kukosekana kwa ukaguzi na majaribio ya injini huko Korea kama ilivyotakiwa na mkataba.

Kwa kivuko cha MV Kazi, baada ya kubadilisha injini nne mwaka 2022, kulikuwa na uvujaji wa mafuta na hitilafu katika injini namba 3 na 4. Hii ilionesha utendaji duni na matengenezo ambayo hayakutosheleza. Ukosefu wa miongozo sahihi ya uendeshaji na matengenezo kutoka kwa mtengenezaji ulichangia hitilafu hizi.






## SURA YA SABA

# UKAGUZI WA UFANISI

## A. UPATIKANAJI WA HUDUMA YA AFYA YA AKILI NCHINI

### 7.1 Ukosefu mkubwa wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii

Huduma za kisaikolojia hazipatikani kwa wakati kwa watu wenye uhitaji na hazijajumuishwa kikamilifu katika mipango, bajeti, na sera za afya. Hii inawaathiri sana wagonjwa wa afya ya akili na makundi mengine yenye mahitaji maalum.



### 7.2 Uhaba wa wataalamu, miundombinu, vifaa tiba, na dawa katika vituo vya afya

Wizara ya Afya haina mpango wa kuajiri wataalamu wa afya ya akili na kusababisha uhaba wa madaktari wa mfumo wa neva na wataalamu wengine. Vituo vingi havipati huduma za utengamo kwa ajili ya kuendeleza ujuzi na kusaidia wagonjwa kupona, ambapo ilibainika kuwa kati ya mikoa 28, ni mikoa mitano tu ndiyo ilikuwa na vituo vya utengamo wa huduma za afya ya akili ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na Kigoma.

## B. UDHIBITI WA VIFAA TIBA KATIKA VITUO VYA AFYA VYA UMMA

### 7.3 Uwepo wa vifaa tiba visivyofanya kazi katika vituo vya afya vya umma

Asilimia 27 ya vifaa tiba vilivyopo havifanyi kazi, na hii imeathiri zaidi kanda ya kati. Hii inasababishwa na ukosefu wa matengenezo na udhibiti duni wa vifaa tiba vinavyoingizwa nchini.

### 7.4 Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba haina kumbukumbu za kutosha za taratibu za usajili wa vifaa tiba

Nimebaini kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) haikuwa na ufanisi wa kuhakikisha uhuishwaji wa vyeti vya usajili wa vifaa tiba. Hii ilipelekea asilimia 51 ya vifaa tiba vilivyosajiliwa kutokulipa ada ya mwaka ya kudumisha usajili.

Matokeo yake, serikali ilipoteza mapato ya Shilingi bilioni 10.26 kwa ajili ya uhuishaji wa vyeti vya usajili wa vifaa tiba na kiasi cha Shilingi milioni 241.04 kwa ajili ya ada ya kudumisha usajili wa vifaa tiba kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23.

## C. UDHIBITI WA MAZAO YA BIASHARA

### 7.5 Udhibiti Mdogo wa Mazao ya Biashara

Ukaguzi ulibaini udhibiti mdogo wa mazao ya biashara, jambo ambalo lilisababisha kupungua kwa mchango wa mazao kama vile tumbaku, chai na korosho kwenye Pato la Taifa. Mifano ya kupungua kwa mchango:

- **Chai:** Mwaka 2022/23, uchangiaji ulipungua kutoka dola za Kimarekani milioni 43.20 hadi dola za Kimarekani milioni 32.30, sawa na kushuka kwa asilimia 26.

- **Tumbaku:** Mchango wa zao la tumbaku ulishuka kwa asilimia 28, sawa na dola za Kimarekani milioni 81.1.

- **Korosho:** Mchango wa korosho ulipungua kutoka dola za Kimarekani milioni 209.1 hadi dola za Kimarekani milioni 139.9 kutoka mwaka 2021/22 hadi 2022/23, sawa na kushuka kwa asilimia 33.

## D. UDHIBITI WA USAMBAZAJI WA MBOLEA

### 7.6 Makisio hafifu ya mahitaji ya mbolea na virutubisho vya mimea

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea haikuwa na mfumo bora wa kukadiria mahitaji ya mbolea nchini. Hii ilisababisha uhaba wa mbolea katika baadhi ya maeneo na ziada katika maeneo mengine. Mamlaka haikuwa na utaratibu madhubuti wa kufuatilia matumizi ya mbolea.

Hii ilisababisha takwimu za mahitaji ya mbolea kuwa kubwa kuliko matumizi halisi. Sababu za utofauti huu ni pamoja na: mfumo duni wa kukusanya takwimu; na uwezo na utayari wa wakulima kununua na kutumia mbolea.

## 7.7 Upungufu wa mbolea yenye ubora

Ukaguzi ulibaini asilimia 14 ya mbolea zilizosajiliwa kati ya Januari na Machi 2021 hazikukidhi viwango. Aidha, mbolea zilisajiliwa kabla ya vipimo vya maabara, na kusababisha mbolea duni kufika kwa wakulima. Hali hii inaweza kupunguza uzalishaji kwa wakulima na kuathiri uchumi wa nchi.




## 7.8 Usambazaji usioridhisha wa mbolea kwa wakulima

Zaidi ya robo (39%) ya wafanyabiashara wa mbolea waliosajiliwa hawakuwapa wakulima mbolea ya ruzuku. Aidha, wakulima asilimia 75 ya wakulima wenye sifa hawakupokea mbolea ya ruzuku. Sababu za kutopokea mbolea hiyo zilijumuisha usambazaji duni, udhibiti hafifu wa bei, na ukaguzi dhaifu wa wauzaji wa mbolea. Matokeo yake, matumizi ya mbolea na uzalishaji wa mazao vilipungua.

## E. UDHIBITI WA ELIMU YA KIUFUNDI NCHINI


### 7.9 Utoaji Usiofaa wa usajili kwa vyuo vya ufundi na walimu

Mfumo wa usajili wa vyuo vya ufundi na walimu una mapungufu makubwa. Hakuna mfumo wa taarifa wa kufuatilia hali ya usajili wa vyuo, na kwa upande mwingine usajili wa walimu wa vyuo vya ufundi umeshuka kutoka asilimia 67 (2019/20) hadi asilimia 56 (2022/23).

Sababu kuu za mapungufu hayo ni pamoja na usimamizi duni wa vigezo vya usajili, kama vile uandikishaji wa wanafunzi wasio na sifa, uhaba wa watumishi wa kitaaluma, na upungufu wa rasilimali za kufundishia. Vigezo visivyo na uhalisia wakati wa ukaguzi na mchakato usiofaa wa utoaji wa ithibati kwa vyuo vya ufundi pia vinachangia tatizo hili.

### 7.10 Mitaala Iliyopitwa na Wakati

Nilibaini kuwepo kwa matumizi ya mitaala iliyopitwa na wakati katika vyuo vya ufundi. Katika mwaka wa fedha 2022/23, asilimia 23 ya vyuo vilivyotembelewa vilikuwa vinatumia mitaala ya zamani ikiwa ni ongezeko kutoka katika asilimia 14 iliyoripotiwa mwaka wa fedha 2020/21.



Sababu za tatizo hili ni pamoja na: (a) Kukosekana kwa barua za ukumbusho (reminder) kutoka NACTVET kuhusu mitaala iliyopitwa na wakati; (b) NACTVET kukosa mfumo wa kufuatilia mitaala inayokaribia kuisha muda wake; na (c) Ufuatiliaji duni na kucheleweshwa kwa uthibitishaji wa mitaala mpya.

## F. USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA WATOA HUDUMA ZA BIMA NCHINI

### 7.11 Ongezeko la Madai ya Bima ambayo hayakulipwa na Kampuni za Bima

Ukaguzi umebaini ongezeko la madai ya bima ambayo hayakulipwa kwa wanufaika na kampuni za bima kati ya mwaka 2019 na 2022. Madai haya yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 114.53 mwaka 2019 hadi Shilingi bilioni 127.253 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 11.

Sababu kuu za ongezeko hili ni pamoja na: kampuni za bima kuchukua muda mrefu sana kulipa madai yaliyoidhinishwa, na kufikia siku 216 katika baadhi ya matukio; na Janga la UVIKO-19 lililosababisha ongezeko la madai ya bima za maisha kwa asilimia 9 na bima za jumla kwa asilimia 3.3.



## G. USIMAMIZI WA UINGIZAJI WA MAFUTA YA PETROLI NA DIZELI NCHINI

### 7.12 Ucheleweshaji wa kuanza kushusha mafuta bandarini umeongezeka kutoka 66% hadi 68% kutoka mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23

Ukaguzi umebaini ongezeko la ucheleweshaji wa kuanza kushusha mafuta kutoka asilimia 66 hadi asilimia 68 kati ya mwaka 2020/21 na 2022/23. Idadi ya meli zilizocheleweshwa kuanza kushusha mafuta kwa siku saba hadi 14 na zaidi ya siku 14 ilikuwa juu katika mwaka wa fedha 2022/23 ukilinganisha na miaka iliyopita. Vikwazo vya miundombinu na kutofuata kwa tarehe iliyopangiwa meli kwa ajili ya ushushaji wa mafuta vilichangia ucheleweshaji huu, na kusababisha kutozwa dola za kimarekani milioni 26.93 kwa sababu ya ucheleweshaji wa kuanza kushusha mafuta ya petrol na dizeli.

### 7.13 Mamlaka ya udhibiti wa huduma za nishati na maji haikubaini kampuni za uagizaji wa mafuta zilizohifadhi mafuta kuweza kutumika kwa muda wa siku 15 wakati wote

Uchambuzi wa Ripoti za mafuta kwa wiki ya 1 na 3 kutoka mwaka 2020 hadi mwaka 2023 zinaonesha kuwa Kampuni za uagizaji wa mafuta ya petroli kati ya asilimia 12 hadi asimilia 62, na Kampuni za uagizaji wa mafuta ya dizeli kati ya asilimia 14 hadi asilimia 65 hazikuhifadhi mafuta ya kuweza kutumika kwa siku 15 kila wakati.

Hii inatokana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutathmini upatikanaji wa mafuta kwa jumla badala ya uhifadhi wa mafuta kwa kila Kampuni ya uingizaji wa mafuta ya petroli na dizeli, hii ilipunguza uwezo wa kutambua kampuni ambazo hazijaweka bakaa ya mafuta inayotakiwa.



# SURA YA NANE

# UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

## 8.1 Madhaifu ya udhibiti katika mifumo ya ukusanyaji mapato

Ukaguzi wangu wa udhibiti katika mifumo ya mapato ya taasisi za umma ulibaini mapungufu kama ifuatavyo:

(i) Mfumo wa **FiRCIS** ulio chini ya Wizara ya Mifugo unaruhusu utoaji wa vibali vya Usafirishaji wa samaki nje ya nchi bila malipo yanayopaswa kufanyika kabla ya utoaji wa vibali hivyo. Pia, mfumo unaruhusu utengenezaji wa bili nje ya moduli stahiki ya mfumo badala yake inatumiwa moduli ya bili mbalimbali ambayo haina udhibiti stahiki kulingana na aina ya bili husika.

(ii) Mfumo wa Uombaji wa Mtandaoni **(OAS)** na **SARIS** inayotumiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) unaruhusu ulipaji wa ada za wanafunzi kwa kutumia namba moja ya ulipaji na kupelekea wanafunzi wengine kudahiliwa bila kufanya malipo, na wengine kutumia namba ya malipo ya wanafunzi wengine kwenye ada na michango mingine.

(iii) Katika mfumo wa **Sage Pastel** inaotumiwa na kampuni ya Magazeti ya Serikali (**TSN)**, mfumo unaruhusu malipo yaliyofanyika mara moja kutumika kuzalisha risiti nyingi za malipo na kulipia ankara mbalimbali za wateja zisizohusiana.

(iv) Mfumo wa **SBMS** unaotumiwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (**TASAC)** unashindwa kukokotoa kwa usahihi ada ana riba zitokanazo na kucheleweshwa kwa malipo ya bili hivyo kupelekea upotevu wa mapato.

(v) Mfumo wa **iCHF-IMIS** unaotumiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kusimamia bima za afya unaruhusu wanachama kupata kibali cha kupewa huduma za afya bila kufanya malipo na kuruhusu baadhi ya wanachama kuendelea kutumia huduma bila kukamilisha malipo.

(vi) Mfumo wa Taarifa za usimamizi wa Biashara ya Kilimo **(ATMIS)** unaotumiwa na Wizara ya Kilimo unashindwa kutambua kama malipo ya bili yanafanywa kwa Shilingi ya Tanzania au dola ya Kimarekani na kusababisha malipo yasiyo sahihi.

(vii) Katika mfumo wa **RRIMS** unaotumiwa na **LATRA**; unatoa vibali vya muda mfupi kwa wateja vikiwa na tarehe isiyosahihi ya kumalizika muda wa matumizi. Hii usababisha leseni zilizopita muda kuonekana kuwa halali. Aidha, kulikuwa na makosa 32 kwenye mfumo kwa ajili ya faini ambapo kiasi kilicholipwa kilikuwa chini ya kiasi kilichotozwa ila mfumo ilizitambua kama zimelipwa kwa ukamilifu.

(viii) Mfumo wa Usajili Mtandaoni (**ORS**) unaotumiwa na TIRA, unaruhusu kutoa leseni moja kwa watoa huduma za bima zaidi ya mmoja.

(ix) Mfumo wa **TAUSI MIS** unaotumiwa na Ofisi ya Rais **TAMISEMI** haudhibiti vifaa vya POS ipasavyo, hivyo kupelekea kuruhusu kukusanya mapato yenye thamani zaidi ya kiwango cha fedha kilichowekwa benki na wakala.

(x) Ukaguzi wa ujumuishaji wa mfumo wa GePG na mifumo ya bili ya Shirika la Posta Tanzania (TPC), Wakala wa Usajili Ufilisi naUdhamini (RITA) na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo Tanzania niligundua tofauti za taarifa za makusanyo baina ya mifumo ya bili na mfumo wa GePG.

## 8.2 Mapungufu ya udhibiti katika mifumo ya kihasibu

### (a) Mapungufu katika mfumo wa uhasibu (MUSE)

Ukaguzi wangu wa udhibiti katika mfumo wa kihasibu wa MUSE ulibainisha mapungufu yafuatayo:

(i) Mfumo unarekodi bili zilizolipwa tu kutoka kwenye mfumo wa GePG na mifumo ya mapato, huku bili ambazo hazijalipwa hazirekodiwi moja kwa moja kwenye mfumo wa MUSE kutoka kwenye mifumo ya mapato, jambo linalosababisha makosa na kutokuwiana katika taarifa za mapato yanayodaiwa.

(ii) Mfumo unaruhusu utengenezaji wa hati za malipo zaidi ya moja kwa masurufu, na mapungufu katika udhibiti wa mgawanyo wa majukumu yanayo sababisha hati za malipo kuanzishwa na kuidhinishwa na mtu mmoja.

(iii) Udhibiti dhaifu unaweza kuruhusu matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa,

(iv) Malipo kwa watoa huduma yanayo rekodiwa moja kwa moja kwenye leja ya mfumo bila kupitia moduli ya manunuzi.

### (b) Mapungufu katika mfumo wa IFMS Epicor wa Bohari ya Madawa (MSD)

Nilibaini udhibiti hafifu katika mfumo wa IFMS Epicor wa Bohari ya Madawa hasa katika kuhakikisha ufanisi kwenye mchakato wa manunuzi. Mapungufu hayo ya mfumo yalipelekea kutofautiana kwa idadi ya bidhaa kati ya mkataba wa ununuzi “Purchase Order” na mahitaji “Purchase Requisition”, kupokea bidhaa bila mkataba wa ununuzi na mahitaji, hati za madai “Invoice” zilizotolewa bila hati ya kupokea bidhaa “Goods Receiving Note” na kutofautiana kati ya hati ya kupokea bidhaa na mkataba wa ununuzi.

### (c) Mapungufu katika mfumo wa ERMS

Ukaguzi wangu ulibainisha mfumo wa ERMS unaotumiwa na taasisi za Umma na kusimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) umeonesha mapungufu katika ripoti inazozitoa, ripoti za utekelezaji wa bajeti na akiba ya mali zilikuwa na taarifa zisizo sahihi.

## 8.3 Haki za utumiaji wa mifumo zilizopitiliza kwa Maafisa wa TEHAMA

Maafisa TEHAMA wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mamlaka TMDA, eGA, Roads Fund Board (RFB) na NSSF walipewa haki za kutumia mifumo ya TEHAMA kinyume na majukumu yao, haki hizo ziliwaruhusu kutekeleza majukumu yasiyo ya kwao kwenye mifumo kama vile kuepuka hatua muhimu katika utoaji vyeti, kutengeneza na kufuta ankara, kutekeleza majukumu ya kihasibu, na afisa rasilimali watu.



## 8.4 Mapungufu katika mifumo ya utumishi na mishahara

Mifumo ya HCMIS (Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) unaruhusu watumishi kupokea mishahara wakiwa likizo ya bila malipo, kupandishwa vyeo bila kukidhi muda wa miaka mitatu ya utumishi, kushushwa vyeo bila mabadiliko ya mishahara na watumishi wenye nambari za utambulisho (check number) zinazofanana. Mfumo wa MIS (Bodi ya Mfuko wa Barabara) na mfumo wa Microsoft Navision (TANAPA) ina mapungufu katika kukokotoa posho na mikopo kwa watumishi. Mfumo wa ERMS (eGA) na PMIS (Shirika la Posta Tanzania) iliruhusu watumishi kupewa likizo nje ya utaratibu.

## 8.5 Mifumo ya TEHAMA inayofanya kazi zinazofanana

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) inatumia mfumo wa ERMS na Sage Pastel kwa shughuli za uhasibu, wakati Mfuko wa Taifa wa Bima ya Jamii (NSSF) ulitengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Mali (AMS) licha ya kuwa na uwezo kama huo katika mfumo wao wa Oracle ERP uliopo. Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatumia mfumo wa MUSE na Sage Pastel kwa ajili ya uhasibu. Vivyo hivyo, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) iliweka mfumo ulioimarishwa wa Uendeshaji wa Bandari (POAS) lakini ikatangaza zabuni kwa Mfumo wa Uendeshaji wa Terminal (TOS) wenye sifa sawa. Zaidi ya hayo, mfumo wa ERMS wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ina moduli ambazo zipo katika mfumo wa manunuzi serikalini wa NeST na mfumo wa rasilimali watu na mishahara wa HCMIS.

## 8.6 Mapungufu ya utendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao

Ukaguzi wa ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ulibaini usimamizi usiojitosheleza katika upatikanaji wa Mifumo ya TEHAMA ambayo tayari ipo katika taasisi zingine za umma, ikisababishwa na kutokuwepo kwa miongozo na taratibu rasmi za Serikali Mtandao, pamoja na uratibu hafifu baina ya taasisi husika. Uwepo wa tozo mbalimbali ambazo zimekuwa kikwazo katika ubadilishanaji wa taarifa baina ya mifumo ya TEHAMA serikalini. Hali kadhalika, idadi ya mifumo iliyounganishwa katika mfumo wezeshi wa ubadilishanaji wa taarifa (GovESB) haijafikia kiwango kinachoridhisha, pia hakuna mkataba wa viwango vya huduma baina ya eGA na taasisi zinazotumia mfumo huo.